



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO



**OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA**

## **TANGAZO**

### **KUTAMBULISHWA KWA KAMPUNI YA TANZANIA MUSIC RIGHTS SOCIETY (TAMRISO) KWA AJILI YA UTOAJI LESENI (UKUSANYAJI WA MIRABAHA) NA UGAWAJI WA MIRABAHA KUTOKANA NA MATUMIZI YA KAZI ZA MUZIKI KATIKA MAENEO YA BIASHARA**

Ofisi ya Hakimiliki Tanzania - COSOTA inapenda kutangazia umma kuwa kufuatia Mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya mwaka 1999 kupitia Sheria ya Fedha Namba 5 ya mwaka 2022 na Kanuni za Hakimiliki na Hakishiriki (Kampuni za Ukusanyaji na Ugawaji Mirabaha), pamoja na Tangazo la Serikali Na. 215 la tarehe 24/3/2023 na *Copyright and Neighbouring Rights (Royalty Collection and Distribution Collective Management Organisations, Government Notice No. 211 published on 24/3/2023*.

COSOTA inajulisha umma kuwa tarehe 21 Julai, 2023 ilitoa leseni ya ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa Kampuni ya Tanzania Music Rights Society (TAMRISO) ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mabadilikio ya Sheria ya kuruhusu kampuni binafsi zinazoanzishwa kwa ajili ya kukusanya na kugawa mirabaha.

Hivyo, jukumu la kukusanya na kugawa mirabaha kwa matumizi ya kazi za Muziki katika maeneo ya biashara litafanywa na TAMRISO kuanzia tarehe 01.07.2023 hadi tarehe 30.06.2024.

COSOTA inawaelekeza Wamiliki wa Vyombo vya Habari, Vyombo vya Usafiri, Baa, Hoteli, Kumbi za Sherehe, Kumbi za Starehe nk, kuwa wanahitajika kulipia leseni ya matumizi ya muziki katika biashara (mirabaha), hivyo watoe ushirikiano kwa kampuni hiyo ili wasanii waendeleo kupokea mirabaha yao na kunufaika na matumizi ya kazi zao. Viwango husika vya makusanyo vitaandaliwa na TAMRISO na wanachama wake na kuidhinishwa na COSOTA kwa ajili ya kuanza kutumika.

**Imetolewa na  
Ofisi ya Hakimiliki Tanzania – COSOTA  
22 Agosti, 2023**